JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS -TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

Namba za simu;
Mkuu wa shule +255753825060
+255620564032
Makamu mkuu wa shule
+255752161569

SHULE YA SEKONDARI ISMANI
S.L.P. 378,
IRINGA.
……

JINA LA MWANAFUNZI …….,
S.L.P ……
……..

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI ISMANI WILAYA YA IRINGA MKOA WA IRINGA MWAKA 2022/2023**

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **Tano** katika shule hii mwaka **2022/2023 tahasusi ya HGL, HKL, HGK, HGE na EGM.**Shule ya Sekondari **Ismani** ipo umbali wa km **42** kaskazini mashariki mwa mji wa Iringa katika Halmashauri ya **Wilaya ya Iringa**.

Usafiri wa basi kutoka Iringa mjini unapatikana stendi ya mabasi ya **mkoa wa Iringa** nauli ya Tsh 2000/= hadi **3000/=**kupitia barabara kuu ya kwenda Dodoma, na kama utatokea Dodoma kuelekea Iringa shuka katika kijiji cha Lwang'a – Ismani Tarafani. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **……** mwisho wa kuripoti ni tarehe **…….**

Mwanafunzi anapaswa kuja na fomu hii ikiwa imejazwa sehemu zote pamoja na picha nne za pasport size.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. SARE.

I. Sketi mbili rangi **nyekundu** mshono wa rinda box yenye marinda isiyobana mwili na iwe ndefu kuishia kwenye enka za miguu (kitambaa kizito.)
II. Mashati meupe mawili ya mikono mirefu.
III. Viatu vyeusi vya **kufunga kwa kamba** na kung'arisha kwa kiwi .(jozi mbili na kuendelea)
IV. Soksi ndefu nyeupe.jozi mbili na kuendelea.
V. Mavazi ya michezo**. (T-shirt za blue2 za Taifa stars na raba nyeusi moja).**
VI. Raba nyeupe
VII. Taulo moja.
VIII. Jozi moja ya kitenge au khanga.
IX. Sweta rangi ya bluu **Shingo V**.
X. Rangi ya ijabu ifanane na sare za shule na hasa shati (kwa wale waislam)
XI. Track suit rangi ya dark blue
XII. Shamba dress gauni rangi ya dark blue (mshono wa solo)
XIII. Skafu (ifanane na kitambaa cha sketi).
XIV. Shilingi elfu 10 kwa ajiri ya t-shirt ya Shule (mwanafunzi atapewa mara afikapo shuleni)

NB: Kwa wale wenye matatizo ya kiafya mfano kifua au pumu waje na puruneki nyeupe.

2.2 Mwanafunzi anaporipoti awe na vitu vifutavyo;

1. Ndoo mbili moja lita **10** na nyingine lita **20 mpya zenye mifuniko.**
2. Jembe moja lenye mpini na kwanja
3. Brash ngumu moja yenye mpini mrefu kwa ajili ya usafi.

4. Mafaili mawili (spring file za Plastic). Kwa ajiri ya kuwekea kumbukumbu muhimu za mwanafunzi na yanapatikana shule kwa shilingi elfu tano (yote mawili)
5. Rimu za karatasi mbili (moja kwa kila muhula)
6. Godoro futi 2 inchi $2^{`1}/_{2}$
7. Mto.
8. Blanketi moja
9. Shuka mbili(rangi ya pinki na blue)
10. Chandarua.
11. Toilet paper
12. Begi la daftari.
13. Daftari (counter book) kuanzia 10.
14. Kamusi ya kiingereza kwa wanaosoma tahasusi za lugha.
15. Scientific calculator kwa wanafunzi wa HGE na EGM
16. Vitabu vya kutosha kulingana na tahasusi (mchepuo) uliopangiwa (tutakagua).
17. Sabuni za kutosha (kufulia na kuogea)
18. Vyombo vya chakula (kontena,kijiko na kikombe)
19. Tochi moja ya betri au ya sola itakayotumika kukiwa na tatizo la mwanga
20. Mahitaji mengine ya kutosha ya mtoto wa kike.
21. Fagio mbili za chelewa.

3.0. ADA NA MICHANGO MINGINE YA SHULE

- ✓ Ada kwa mwaka 70,000/= (35,000/= kwa muhula.)
- ✓ Taaluma 25,000/ inalipwa mara moja tu.
- ✓ Ukarabati wa samani 20,000/= inalipwa mara moja tu.
- ✓ Kitamburisho na picha 6,000/= inalipwa mara moja tu.
- ✓ Wapishi, walinzi na vibarua wengine 40,000/= (20,000/= kwa muhula.)
- ✓ Nembo ya shule 2000/-
- ✓ Bima ya afya na huduma ya kwanza 10,000/=
- ✓ Huduma ya umeme 10,000/=
- ✓ Fedha ya tahadhari 5000 (haitarudishwa)

Jumla ya ada na michango mingine kwa mwanafunzi ni shilingi 188,000/=(muhula wa kwanza 133,000/= na 55,000/= tu muhula wa pili)

ZINGATIA: Ada na michango yote iingizwe benki kwenye akaunti namba ya NMB **60501200081**, j**ina la akaunti ni Ismani Sekondary school.** Andika jina la Mwanafunzi kwenye karatasi ya benki ya malipo (**BPS**).

VITABU PENDEKEZWA.

KISWAHILI

1. Saluhaya C.M(2016): Nadharia Ya Lugha Kidato Cha Tano, Sita Na Elimu Ya Juu(toleo la pili. Ahmadiyya printers, Ya dare s sallam Tanzania
2. Saluhaya C.M (2012): Nadharia Ya Tahakiki Fasihi Ya Kidato Cha Tano Na Sita.
3. KILANGI . E. L (2019) NADHARIA YA FASIHI,KIDATO CHA 5 na 6
4. KILANGI .E.L (2019) TAHAKIKI KIDATO CHA 5 na 6
5. KILANGI .E.L (2019) NADHARIA YA LUGHA,KIDATO CHA 5 na 6

HISTORY

1.Salehe Yasini(2016):Essentials In Advanced Level History Paper2, Ahmadiyya printing press.

2. Shibitali c.k(2017): contemporary historical events , advanced level history 1, 3rd ED

3.Mwl. Bakari Madaya (2018): History paper one Lesson notes for Advanced Certificate of Secondary education. Based on the current Tanzania syllabus(2010)

GEOGRAPHY

1.David Waugh (2009): An integrated approach, 1010printing international ltd china.

2.Richard white (1984): African in focus, a physical human and economic geography.

3.C.R. Kothari (2008): Research methodology, new age International (p) limited publishers.

4.TIE (2016) GEOGRAPHY FOR SECONDARY SCHOOLS –FORM FIVE

ECONOMICS

1.C.M. Ambilikile ( ):Economics for Advanced and Professional Studies
2.Zist kamili( ): Economics for High Schools and Commercial Schools
3.N.S. SALEEMI(): Modern Economics.

ENGLISH LANGUAGE

1. LINGUISTIC CONCEPTS FOR ADV. LEVEL ENGLISH LG ONE BY JULTON SANGA (2017)
2. A RECOMMENDED ENGLISH LITERATURE HAND BOOK FOR A-LEVEL STUDENTS BY PASCHAL SALAWI 2014, 2015
3. ANALYTICAL ANALYSIS OF ADVANCED LITERATURE ENGLISH LANGUAGE FORM 5 & 6 BY MGONJA M. E (2019) First Edition.
4. ADVANCED LEVEL ENGLISH A PRACTICAL APROACH BY NICHOLAUS ASHELI (2014) Third edition

MATHEMATICS

1.SEPTINE I. SILLEM (2005): ADVANCED MATHEMATICS, 1ST ED, FORM FIVE
2.SEPTINE I. SILLEM (2015): ADVANCED MATHEMATICS. 1ST ED, FORM SIX

BASIC APPLIED MATHEMATICS

3. TANZANIA INSTITUTE OF EDUCATION (2019): Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools Student's Book**. Form Five and Six.**

GENERAL STUDIES

4. Mbalase. R, Richard( ): General Studies For Advanced Level Certificate Form Six And Form Five.

4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII (ZITEKELEZWE NA MWANAFUNZI)

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima,
b) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation),
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa hapa shuleni,
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii,
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule,
f) Kuvaa sale ya shule wakati wote unapotakiwa,
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
h) Kutunza Mali za umma.
i) Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele.
j) HURUHUSIWI KUJA NA SIMU SHULENI

4.1. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha ,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya kusimamia elimu nchini na Ofisi ya RAIS –TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shule kwa kuwa yanaweza kusababisha ufukuzwe shule au adhabu kali.

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 mfululizo bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako ,walimu,walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana ,kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
vi. Ulevi na unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
vii. Uvutaji wa sigara.
viii. Mahusiano ya kimapenzi.
ix. Kuolewa .
x. Kutoa mimba au kupata mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uharifu,siasa na matendo yeyote yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kukutwa,kumiliki au kutumia simu au kadi ya simu .
xiv. Kudharau bendera ya taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua ama kutishia kujiua.
xvi. Kuharibu mali za umma kwa makusudi

Nb.Mawasiliano ya mwanafunzi na Mzazi/Mlezi yafanyike kwa simu ya shule namba: 0744004215 na 0658735390 (jumatano jioni na jumamosi tu)

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

MWASOMOLA C

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI ISMANI

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA TANO.

(Sehemu ya kwanza ya fomu hii ijazwe na Mwanafunzi na sehemu ya pili ijazwe na Mzazi au Mlezi)

SEHEMU YA KWANZA

(Sehemu hii ijazwe na Mwanafunzi mwenyewe)

picha

Mimi …….. (Mwanafunzi) kwa hiari yangu nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Ismani. Aidha naahidi kutoshiriki/kutoanzisha migomo, fujo, kufuata sheria na kufanya makosa ya jinai.

Jina la Mwanafunzi ……

Sahihi ya Mwanafunzi …….

Tarehe …./…../20….

SEHEMU YA PILI

(Sehemu hii ijazwe na Mzazi/Mlezi)

Mimi …….. Mzazi/Mlezi wa ……..……..
Nakubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda WOTE awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa Walimu, Wazazi, Viongozi na Jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote za shule. Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote za shule hadi atakapo maliza shule.

Jina la Mzazi/ Mlezi …….

Sahihi …….

Tarehe …/…/20…..

OFISI YA RAIS TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI ISMANI
FOMU YA KUKIRI KUKUBALI SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE
HABARI ZA MZAZI/ MLEZI
(Fomu hii ijazwe na Mzazi /Mlezi)

1. Jina kamili la baba……
2. Uraia ……
3. Kazi yake ……..
4. Jina kamili la mama ……
5. Uraia ……..
6. Kazi yake ……..
7. (Jina kamili la mlezi (iwapo haishi na wazazi wake) ……

kazi na anuani ya mzazi/mlezi ……

8. Mtoto anaishi na Baba tu, Mama tu, Wazazi wote au Mlezi (kata yasiyohusika).
9. Dini ya mzazi/Mlezi…….
10. Dhehebu …….
11. Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa

likizo……

12. Mimi …… Mzazi/Mlezi wa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi, na mwenye bidii.

…… ……
Tarehe Saini ya Mzazi/Mlezi

MEDICAL EXAMINATION FORM

(**To be completed by medical officer in respect of all new students**)

Full name ……..

Age ……

1. Blood count (red and white) ……
2. Urine examination …….
3. Stool examination ……
4. Syphilis …….
5. T.B Test ……
6. Ear test …….
7. Eye test ……
8. Spleen ……..
9. Pregnancy test ……
10. Abdomen ……
11. Additional information or any other Physical, Mental, Hereditary of infectious diseases
    ……
    ……

Treatment after examination

……
……..

MEDICAL CERTIFICATE

I certificate that the above concerned has been examined and found fit into pursue for further education.

Signature ……

Designation ……..

Station …….

(Official stamp)

Date …./…./20…

NB: fomu hii ijazwe na Mganga katika Hospitali inayotambulika na serikali.